

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**



**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI SEKTA YA AFYA NA MAENDELEO YA  
JAMII KWA NAIBU WAZIRI WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO**

**KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 HADI DESEMBA 2017**

*Imetayarishwa na:-  
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S.l.p 28001  
Kisarawe*

*Desemba 2017*

# **1. TAARIFA YA UTEKELEZAJI SEKTA YA AFYA NA MAENDELEO YA JAMII KWA KIPINDI CHA 2016/17 HADI DESEMBA 2017**

## **1.0 Utangulizi**

Wilaya ya Kisarawe ni miongoni mwa Wilaya 8 na Halmashauri 9 zilizoko Mkoa Pwani. Wilaya imegawanyika katika Tarafa nne (4) ambazo ni Sungwi, Maneromnago, Mzenga, na Cholesamvula. Aidha zipo Kata 17 na vijiji 66. Aidha, Wilaya ina vitongoji 216 vya vijijini na 19 vya Mamlaka ya Mji Mdogo.

## **Eneo la Wilaya**

Wilaya ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 3,535 na ipo mita 1,000 juu ya usawa wa bahari.

## **Idadi ya Watu**

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, wakati huo wilaya ilikuwa na jumla ya watu 101,598 (wanawake 50,967 wanaume 50,631). Makadario ya sasa Wilaya ina jumla ya watu 114,054 ambapo wanawake ni 57,216 na wanaume ni 56,838. Wastani wa watu kwa kaya ni 4.3. Ongezeko la watu ni wastani wa 2.1% kwa mwaka.

## **Muundo wa Wilaya Kiutawala**

Kiutawala Wilaya imegawanyika katika tarafa 4 za Sungwi, Maneromango, Mzenga na Cholesamvula. Ina kata 17 na vijiji 66 vilivyoandikishwa kisheria. Kutokana na tangazo la serikali Wilaya sasa imekuwa na mamlaka ya mji mdogo wa Kisarawe wenye Kata nne ambazo ni Kisarawe, Kazimzumbwi, Msimbu na Kiluvya. Hatua iliyofikiwa, Mamlaka imeshapata wenyeviti wa vitongoji, Mwenyekiti na makamu na kamati tatu za mamlaka.

## **2.0 Watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii**

Idara ya Maendeleo ya Jamii ina jumla ya watumishi 22; wanaume 5 na wanawake 17. Kati ya watumishi hao 3 wameazimwa kufanya kazi katika idara nyingine na TAMISEMI, Mmoja (1) ni Mratibi wa UKIMWI, wawili (2) wako TASAF. Aidha watumishi 9 wako ngazi ya kata. Kulingana na idadi ya Kata zilizopo 17 idara ina upungufu wa watumishi 8 kwa ngazi ya Kata.

Vilevile Idara hii ni kiungo cha mahusiano inayofanya uraghibishi kwa jamii katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ili kuondokana na utegemezi, umaskini na kutumia fursa

ya rasilimali zilizopo katika kujiletea mabadiliko chanya ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Idara ina madawati manne (4) ambayo ni dawati la jinsia na watoto, dawati la takwimu, utafiti na mipango vijijini, dawati linaloratibu shughuli za asasi za kiraia (NGOs, CBOs, na FBOs), na dawati la vijana. Aidha, idara hii inasimamia miradi miwili ya TASAF na UKIMWI ambapo waratibu wa miradi hiyo ni Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa mujibu wa miongozo ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii ilitokeleza shughuli mbalimbali za uwezesaji wananchi kiuchumi kwa kushirikiana na wadau wengine wa Maendeleo (*Taasisi wezeshi zinazofanya kazi na Baraza la uwezesaji wananchi kiuchumi – NEEC*)

### **3.0 Shughuli zilizotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha 2016/17 – Desemba 2017**

Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Sera, Sheria, Kanuni na maelekezo mbalimbali toka Serikalini Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii tumeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kuwawezesha wananchi kiuchumi. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

#### **3.1 Uwezesaji Wananchi kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF), Vijana (YDF), na Walemavu.**

Katika kuteleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 (*Ukurasa wa 110 hadi ukurasa wa 118*), Sera ya Maendeleo ya Jamii 1996, Sera ya Wanawake na Maendeleo ya Jinsia ya Mwaka 2000, Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 na kuendeleza dhana ya kushiriki kukuza uchumi wa viwanda; Halmashauri ya wilaya imeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa namna mbalimbali. Moja ya uwezesaji huo ni kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani na kutoa mikopo yenye riba nafuu na kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na walemavu vinavyojishughulisha na shughuli za uzalishaji mali (Ujasiriamali na biashara ndogo ndogo) kupitia viwanda vidogovidogo. Ambapo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 Halmashauri ya wilaya ilitenga kwenye bajeti kiasi cha shilingi **140,000,000/=** kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake na

vijana 80 lakini ilitoa mikopo yenye riba nafuu kiasi cha shilingi **100,550,000/=**sawa na asilimia **71.8 %** kwa vikundi vya wanawake na vijana 75 vyenye wanachama 738.

Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi milioni sabini na tatu (73,050,000/=) kilikopeshwa kwa vikundi vya wanawake **61** vyenye wanachama **623** na kiasi cha shilingi **27,500,000/=** kimekopeshwa kwa vikundi **14** vya vijana vyenye wanachama **115**.

Aidha, kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi Milioni thelathini na moja (31,000,000) ni kutoka Serikali kuu ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto walitoa mkopo kwa Halmashauri wa shilingi **20,000,000/=** kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) na kiasi hicho cha fedha kilikopeshwa kwa vikundi vya wanawake **15** vyenye wanachama 150. Pia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu walitoa Mkopo kwa Halmashauri kiasi cha shilingi **11,000,000/=** kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF).Fedha hizo zilikopeshwa kwa vikundi vya vijana 3 vyenye jumla ya wanachama 16.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 (*Kuanzia Julai 2017 hadi Oktoba 2017*) Halmashauri imetenga bajeti ya 10% ya mapato ya ndani ambayo ni Jumla ya shilingi **220,000,000(150,000,000 – WDF + 70,000,000 - YDF = 220,000,000/=)** ili kukopesha jumla ya vikundi **100 (70 vya wanawake na 30 vya vijana)** vya wanawake na vijana.

Mpaka Novemba 2017 jumla ya vikundi 49 vya wanawake, vijana na walemavu vyenye wanachama **411** vimepewa mikopo yenye masharti nafuu yenye jumla ya shilingi **102,204,000/=** sawa na asilimia 46 sawa (Mikopo hii imetolewa mwezi Novemba 2017)

***(Kiambatanisho ‘B’)***

Kati ya vikundi hivyo; vya wanawake ni 41 vilivyokopeshwa mikopo yenye thamani ya shilingi **73,500,000/=**, vikundi vya vijana ni 7 vilivyopewa mikopo yenye thamani ya shilingi **26,704,000/=** na kikundi kimoja cha walemavu (1) kilichokopeshwa mkopo wa shilingi **2,000,000/=**

***Aidha kati ya vikundi 49 vilivyokopeshwa mikopo vikundi 12 vinajighulisha na uzalishaji wa bidhaa kupitia viwanda vidogo vidogo***

### **3.2 Kuhamasisha Jamii kuanzisha Vikundi vya Uzalishaji Mali na kuvisajili.**

Wilaya ina jumla ya vikundi vya uzalishaji mali vilivyotambuliwa 4,627 vyenye jumla ya wanachama 33,256. Kati ya vikundi hivyo 643 vimepata usajili Halmashauri sawa na asilimia 14%

#### **a) Vikundi vya Wanawake**

Wilaya ina jumla ya vikundi 295 vya wanawake ambavyo hujishughulisha na uzalishaji wa bidhaa kupitia viwanda vidogo vidogo kama vile utengenezaji wa batiki,wine, usindikaji wa matunda na mbogamboga,korosho,asali,utenegenezaji wa

viatu, vingine vinashughulika na ufugaji, bustani,migahawa (Mama Lishe) , na kilimo. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya vikundi 95 vyenye wanachama 770 vya wanawake viliweza kusajiliwa ngazi ya Wilaya.Aidha kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Novemba 2017 jumla ya vikundi vya wanawake 50 tayari vimesajiliwana vikundi 150 tayari vimetambuliwa na vinahamasishwa ili visajiliwe.

#### **b) Vikundi vya Vijana**

Wilaya ina jumla ya vikundi 130 vya vijana wanaojishughulisha na shughuli za useramala, mapishi na mapambo, ushonaji wa nguo, ufundi, umeme, gereji, usafirishaji (Bodaboda), uchongaji wa vinyago, kilimo, ufugaji na shughuli nyinginezo. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya vikundi **68** vya vijana viliweza kusajiliwa ngazi ya Wilaya.Na kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Novemba 2017 jumla ya vikundi vya vijana 40 tayari vimesajiliwa, na vikundi 22 vimetambuliwa na vinahamasishwa ili visajiliwe.

#### **c) Vikundi Mchanganyiko**

Kuna jumla ya vikundi mchanganyiko 275 Vikundi hivi ni vya wazee, watu wa makamu, wanaume na wanawake na wanajishughulisha na kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo na shughui nyingine za uzalishaji mali. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya vikundi **125** vya mchanganyiko viliweza kusajiliwa ngazi ya Wilaya. Na kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Novemba 2017 jumla ya vikundi mchanganyiko 62 tayari vimesajiliwa.

#### **d) Vikundi vya Kuweka Akiba, Hisa na Kukopeshana (VICOBA)**

Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tumeweza kuhamasisha jamii kujiunga katika vikundi vya kuweka Akiba, Hisa na kukopeshana (VICOBA) ambapo jumla ya VICOBA 3,927 vimeanzishwa. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya VICOBA 345 vilisajiliwa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Novemba 2017 jumla ya VICOBA 48 vimesajiliwa ngazi ya Wilaya. Jumla ya VICOBA 393 vimesajiliwa sawa na asilimia 10 na VICOBA 3,534 bado havijasiliwa.

*Pia kati ya vikundi vilivyotajwa hapo juu jumla ya vikundi 32 vinajishughulisha na shughuli za uzalishaji bidhaa kupitia viwanda vidogo vidogo.*

#### **3.3 Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs/FBOs, INGOs)**

Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe imekuwa ikitekeleza Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 kwa kushirikiana na Mashirika/Taasisi zisizo za Kiserikali (AZISE) katika kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo na za kijamii ikiwa ni pamoja na kusaidia kuchangia utoaji wa huduma za afya kama vile kusaidia kuhamasisha jamii kupinga vita dhidi ya maradhi ya Malaria, UKIMWI n.k, ujenzi wa zahanati, lishe kwa watoto mashuleni, ulinzi na usalama kwa watoto, utetezi wa haki za wanawake na kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia, kuchangia katika kutoa huduma ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, huduma ya maji vijijini, kuwawezesha wananchi kiuchumi, na kuchangia kufanikisha sherehe za Kitaifa na maadhimisho mbalimbali kama vile sherehe za Maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani, siku ya mtoto wa Afrika, Siku ya Vijana Dunia, siku ya mtoto wa kike, sherehe za mbio za mwenge na kusaidia kutoa Elimu ya masuala ya sheria, utawala na uhamasishaji jamii katika masuala uhifadhi wa mazingira.

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi Novemba 2017 Rejista ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inaonyesha kuwa na idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yapatayo 81, ambayo yaliwahi kuomba na kujitambulisha kutekeleza miradi mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Baada ya msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutangaza kuhakiki Mashirika yote yasiyo ya kiserikali kuanzia tarehe 21 hadi 31 Agosti 2017 kwa lengo la kuhuisha orodha ya mashirika

yasiyo ya Kiserikali nchini, kuboresha data na kupima utekelezaji wa majukumu ya mashirika haya. Jumla ya mashirika 16 yasiyo ya kiserikali yalijitokeza kuomba kupatiwa barua ya utambulisho kwenda kwa Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya uhakiki, idadi hiyo ni ndogo sawa na asilimia 20 tu ya mashirika 81 yaliyopo katika rejista ya NGOs katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe

Hata hivyo, Serikali imeamua kuongeza muda wa miezi miwili ya uhakiki wa mashirika yasiyo ya Kiserikali nchini kutokana na kushindwa kufikia hata nusu ya mashirika yaliyotarajiwa kuhakikiwa kwa kipindi cha mwezi mmoja wa uhakiki.

### **3.4 Elimu ya Ujasiriamali na Biashara**

Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tuliendesha makongamano matatu kwa wanawake na vijana wajasiriamali katika Kata za Kisarawe, Mzenga, Kazimzumbwi, Masaki, Kiluvya na Msimbu ambapo jumla ya washiriki 5,385 waliweza kushiriki katika makongamano hayo. Katika makongamano hayo taasisi wezeshi zinazotambuliwa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kama vile PPF, TRA, PSPF, LAPF, DCB, TPB, TBS, TFDA, SIDO, NMB, BRELA na wengine walialikwa na kutoa mada mbalimbali zinazolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi.

### **3.5 Kujengea uwezo, kufanya tathmini na ufuatiliaji wa vikundi vya wanawake na vijana.**

Idara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikivitembelea vikundi vya wanawake na vijana kwa malengo ya kuvifanyia tathmini vikundi vilivyoomba mikopo na kuvijengea uwezo. Kabla ya vikundi kupatiwa mikopo vimekuwa vikijengewa uwezo katika nyanja za uongozi wa kikundi, utunzaji wa kumbukumbu za biashara, uwekezaji, na uandikaji wa taarifa za shughuli za kikundi na urejeshaji wa mikopo.

Aidha Idara imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa marejesho vikundi vilivyokopeshwa mikopo kwa awamu mbalimbali. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 jumla ya vikundi 75 vya vijana na wanawake vimeweza kutembelewa na kufanyiwa tathmini kabla ya kupewa mikopo, kujengewa uwezo na kuhamasisha marejesho ambapo jumla ya shilingi 57,000,000/= zilirejeshwa na vikundi vilivyokopeshwa mikopo hapo awali.

### **3.6 Kukiwezesha kikundi cha Sauti ya wanawake Kazimzumbwi (VOWEK) jiko la kiwanda cha kutengeneza mikate.**

Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Asasi ya Chole Center for Poverty Alleviation (CCPA) na Shirika la Rural Urban Development Initiative (RUDI) imekiwezesha kikundi cha VOWET kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza mikate kwa kutumia jiko linalotumia nishati ya juu. Mradi umegharimu shilingi

Milioni Arobaini (**40,000,000/=**) Aidha kikundi kimepewa mafunzo na kujengewa uwezo wa kuendesha mradi huo.

### **3.7 Kuanzisha SACCOS ya Wanawake ya Wilaya ya Kisarawe.**

Halmashauri ya Wilaya kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii imewahamasisha wanawake kuanzisha SACCOs ya Wanawake ya Wilaya. Wanawake wamehamasika kuunda SACCOs yao na wameanza kulipa viingilio, kununua hisa, na kuweka akiba. Tayari wameishapeleka maombi ya usajili kwa mrajis wa vyama vya ushirika kwa ajili ya usajili. Hadi kufikia Novemba 2017 walikuwa na mtaji wa shilingi **3,743,000/=**.

### **3.8 Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani na Vijana**

Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tuliandaa na kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8/03/2017 ambapo yaliadhimishwa Kimkoa katika Wilaya ya Kisarawe, Kata ya Kisarawe na vikundi mbalimbali vya wanawake walipata fursa ya kuonyesha bidhaa mbalimbali wanazotengeneza kupitia viwanda vidogovidogo na kuuza.

Kauli mbiu ya Mwaka huu 2017 iliyokuwa inasema **“Tanzania ya Viwanda.” Wanawake ni Msingi wa Mabadiliko ya Kiuchumi**” na iliwafikia walengwa kwa asilimia 85% hii ni kutokana na idadi kubwa ya wanawake na wananchi waliojitokeza na kuhudhuria maadhimisho hayo ambapo jumla ya washiriki **1,050** walihudhuria.

Siku hiyo ya kilele Mgeni Rasmi alikabidhi Hundi ya mfano yenye thamani ya kiasi cha **Tshs.61, 550,000/=** kwa vikundi vya Wanawake 38 na Vijana 11 ikiwa ni Mikopo kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) na Vijana (YDF). Aidha tuliadhimisha siku ya vijana Duniani iliyokuwa na kauli mbiu ya **“Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana katika kudumisha Amani”**. Maadhimisho hayo yalifanyikia Kata ya Marumbo na Mgeni Rasmi alikabidhi mifuko



thelathini (30) ya saruji iliyotolewa na Kiwanda cha Saruji cha Kisarawe (*Kisarawe Lucky Cement*) kwa kikundi cha Vijana cha Seven Young kilichopo katika Kijiji cha Msegamo Kata ya Maneromango. Jumla ya vijana 205 (Me 97 na Ke 108) walishiriki maadhimisho hayo.

### **3.9 Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za vijana**

Halmashauri inaendelea kutekeleza agizo la Mh. Rais la kutenga maeneo ya uzalishaji mali kwa ajili ya shughuli za vijana, hadi kufikia Juni 2017 ekari 533 zilikuwa zimetengwa katika Kata 6 na vijiji 21

Pamoja na hayo Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama vile mashirika yasiyokuwa ya kiserikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa watoto wa kike wanalindwa na kupatiwa haki zao za msingi bila kujali kuwa ni watoto wa kike kama ilivyo kuwa hapo nyuma kuwa mila na desturi kandamizi kwa mtoto wa kike hivyo Halmashauri kushirikiana na wadau imejitahidi kupunguza mila hizo na hii imepelekea mtoto wa kike kupata huduma bora kama , lishe bora, kucheza na kupumzika, haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi na haki ya kuishi, pia Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi **9,200,000/=** katika bajeti yake ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya Taulo za kike (Ped) ili kumuwezesha mtoto wa kike asome vizuri

Halmashauri inasimamia na kutekeleza kwa vitendo Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 na sheria nyingine kama vile sheria ya ndoa, ajira, kuasili na makosa ya jinai ambazo zinamlinda mtoto wa kike katika majanga na vitendo viovu.

Lakini baadhi ya wazazi, walezi na jamii na wananchi kwa ujumla wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa watoto wa kike na kuwafanyisha kazi nyingi kama vile malezi na usimamizi wa nyumba, kuwaozesha watoto wa kike wakiwa bado shuleni, kukataa kuwasomesha watoto wa kike, kufanyiwa vitendo vichafu kama vile kubakwa, na kulawitiwa hali ambayo husababisha kupata mimba pamoja na magonjwa makubwa ya kuambukiza kama vile gonjwa hatari la **UKIMWI**. Pia wengine hujiingiza katika matumizi na biashara ya madawa ya kulevyva.

Katika kupambana na hali hii Halmashauri imeimarisha mifumo ya Ulinzi na Usalama. wa Mtoto ambapo imeanzisha Timu ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto ya Wilaya (DCPT) na Wilaya yetu ya Kisarawe katika Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa Wilaya pekee iliyo na mahakama ya mtoto kuhakikisha kuwa haki za watoto hususani wa kike zinalindwa.

Pamoja na jitihada zote hizo zinazofanywa na Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo bado inasikitisha kuona kuwa kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 mpaka sasa jumla ya wanafunzi wa kike 9 katika shule za msingi wameripotiwa kupata mimba na wanafunzi wa kike 26 toka Shule za Sekondari wameripotiwa kupata mimba na wengine 136 kuacha kuendelea na masomo yao kutokana na sababu mbalimbali.

### **3.10 Mradi wa Kunusuru Kaya Masikini – TASAF III**

Mradi wa kunusuru kaya masikini ulizinduliwa rasmi mwezi Novemba 2014 kwa kutambua walengwa katika vijiji 56 katika Wilaya yetu ingawa utekelezaji uliendelea kwa vijiji 49 na vijiji vingine saba viliachwa kwa ajili ya kufanyiwa tafiti mbalimbali.

Aidha katika mwaka wa fedha 2016/2017 TASAF pia ilitekeleza miradi ya ajira za muda kwa kaya masikini 43 katika vijiji 43 vilivyoingia kwenye mpango huu kati ya vijiji 49.

Kwa kipindi cha kuanzia Septemba 2015 hadi Novemba 2017 mpango wa kunusuru kaya masikini umekwisha toa kiasi cha shilingi **846,940,000/=** ikiwa ni fedha za ruzuku na kiasi cha shilingi **186,180,400/=** ikiwa ni fedha kwa ajili ya malipo ya ajira za muda.

Hivyo kwa mwaka 2017/2018 TASAF inaendelea na shuhuli zake ambapo miradi 52 imeibuliwa kwa kipindi hiki na itaanza kutekelezwa hivi punde.

#### **Mafanikio Yaliyofikiwa:-**

- i. Katika kipindi hiki ambapo walengwa wanapokea ruzuku zao kaya lengwa zimekuwa na uhakika wa chakula
- ii. Mahudhuruio ya wanafunzi yameongezeka kwa kaya zile ambapo vijiji vyao vipo katika mpango wa Kunusuru Kaya Masikini.
- iii. Baadhi ya walengwa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) – ambapo jumla ya wanufaika **1,051** wa mpango wa TASAF III wamejiunga na CHF
- iv. Baadhi ya walengwa kunzisha ufugaji mdogo mdogo wa mbuzi, kuku nk
- v. Walengwa kuendelea kuboresha makazi yao ikiwemo ununuzi wa bati na saruji

## Changamoto

- i. Ucheleweshaji wa fedha za ajira za muda
- ii. Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya ajira za muda hali iliyopelekea miradi mingi kutekelezwa kipindi cha mvua
- iii. Wasimamizi wa miradi ya ajira za muda (LSP) kutopata mafunzo ya kutosha
- iv. Kutokuwepo kwa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa baadhi ya viongozi wa vijiji

### 3.11 Kupunguza maambukizi ya V.V.U, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI

Kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2017 Halmashauri kupitia kitengo cha UKIMWI ilitoa mafunzo ya mwitikio usio wa kitabibu kwa Kata 15. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Kamati za UKIMWI sehemu za kazi ngazi ya Kata ambapo wajumbe 24 walipatiwa mafunzo hayo. Vilevile mafunzo ya kujikinga na maambukizi mapya ya V.V.U yametolewa kwa watu 365 (Me 173 na Ke 172) katika Kata ya Msimbu kwa njia ya sanaa. Pia upimaji wa V.V.U umefanyika na watu **6457 (Ke 3727, Me 2730)** katika vituo vya Afya watu 6,272 walipima (Ke 3,641 na Me 2,631) na waliokutwa na maambukizi ni 256 (Ke 162 na Me 94) na upimaji wa V.V.U katika mikusanyiko mikubwa ya watu ambapo siku ya Zaramo festival *“Tamasha la Kuenzi Tamaduni za Kizaramo”* watu 185 (Ke 86 na Me 99) walipima V.V.U na hakuna aliyekutwa na maambukizi.

Aidha kwa kipindi tajwa jumla ya kondomu 1,800 ziligawiwa kwa makundi mbalimbali ya wananchi.

Kuwasaidia watu wanaoishi na V.V.U jumla ya watu 87 (Me 33, Ke 54) walipewa chakula. Watu 63 kati ya 87 walikuwa na utapiamlo mkali na 24 walikuwa na utapiamlo wa kadri. Kwa kipindi cha 2016/2017 mafunzo mbalimbali kuhusu UKIMWI yalifanyika. Baadhi ya mafunzo hayo ni:-

Mafunzo ya kuzuia Maambukizi mapya ya UKIMWI na V.V.U na stadi za maisha yalitolewa kwa wanafunzi wa Sekondari wapatao 965 (Me 416, Ke 549) toka Shule za Sekondari za Vikumburu, Maneromongo, Gongoni, Janguo, Chole, Gwata, Overland na The Great lake. Vilevile mafunzo ya kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kwa vijana 37 (Me 27, Ke 10) walio nje ya shule kwenye kata 7 za Mafizi, Mzenga, Kisarawe, Kazimzumbwi, Msimbu, Masaki na Maneromongo yalitolewa

Aidha, mafunzo kuhusu UKIMWI na madawa ya kulevya yalifanyika katika Kata ya Kazimzumbwi, Masaki, na Kisarawe Kutoa mafunzo kwa kamati ya kudhibiti ukimwi ngazi ya kata ambapo jumla ya wajumbe 24 (Me 10,Ke 14) walipatiwa mafunzo.

### **3.12 Uhamasishaji wa Mkakati wa Utekelezaji Maendeleo ya Sekta ya Maji Vijijini**

Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe katika kutekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Vijijini, kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Idara ya Maji tumeweza kuanzisha mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji kwa kuwezesha kuunda na kusajili vyombo huru vya watumia maji (JUMUIYA ZA WATUMIA MAJI - COWSOs) katika vijiji 21 viliyojengewa miradi ya maji kwa kutumia rasilimali fedha toka mapato ya ndani ya Halmashauri, ruzuku toka Serikali kuu, ufadhili wa Benki ya Dunia (WB), Jamhuri ya watu wa China, Falme za Kiarabu na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kama vile Shirika la Plan International, Shirika la Dawasco, na Shirika la Global Alliance.

Kazi ya uundaji wa vyombo huru vya watumia maji inakwenda sambamba na mchakato wa kuwashirikisha wananchi kupitia mikutano maalumu ya vijiji, kufanyika kwa usaili wa kuwapata wajumbe wa bodi, kuwapatia mafunzo ya kuwaandaa, kusimamia na kuendesha miradi ya maji katika vijiji husika. Pamoja na jitihada hizo zilizofanywa kuanzisha vyombo vya watumia maji bado Jumuiya za watumia maji zinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya Changamoto hizo ni:-

- i. Baadhi ya viongozi wa Bodi na watendaji wa miradi ya maji kuwa na uelewa mdogo hali inayopelekea kushindwa kukabiliana na changamoto katika kusimamia na kuendesha miradi ya maji ikiwamo kushindwa kufuata maelekezo na miongozo waliyopatiwa wakati wa mafunzo.
- ii. Jamii kuwa na mwamko mdogo hasa watumia maji katika kuhudhuria mikutano na kushiriki kufanya maamuzi na kuweka maazimio mbalimbali kuhusu miradi ya maji katika vijiji/vitongoji vyao.
- iii. Hali ya migogoro ya mara kwa mara baina ya wajumbe wa Halmashauri za vijiji/Vitongoji dhidi ya wajumbe wa bodi. Migogoro hiyo huathiri mashirikano katika

kusimamia na kuendesha miradi ya maji, hasa katika kuhamasisha jamii kuchangia 2.5% na baadhi ya wajumbe wa Bodi kujiuzulu.

#### **4.0Changamoto Mbalimbali Zinazoikabili Idara ya Maendeleo ya jamii**

Idara ya Maendeleo ya Jamii pamoja na kutekeleza majukumu yake ya kila siku lakini inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazopelekea kutofikia baadhi ya malengo. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

- i. Uhaba wa rasilimali fedha na rasilimali watu hali inayopelekea kutowafikia wananchi walio wengi zaidi kutoka vijiji vya pembezoni na wakati mwingine kupelekea kushindwa kufuatilia mpango kazi wa idara. *(i.e Kutopata ruzuku toka Serikali kuu kwa mujibu wa bajeti inayopangwa)*
- ii. Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 8 ngazi ya kata
- iii. Uhaba wa vitendea kazi kama vile usafiri, pikipiki n.k
- iv. Watoto wengi kulelewa na Bibi/Babu – wazazi wao huwaacha na kwenda kutafuta maisha Dar eS Salaam hali inayopelekea watoto hao kutozingatia kwenda shule na kujikita zaidi kutafuta pesa ili kuitunza familia.
- v. Kukosa masoko ya uhakika kwa ajili ya bidhaa wanazotengeneza kama vile batiki, sabuni za unga na maji. Aidha baadhi ya vikundi havina maeneo maalumu kwa ajili ya kufanyia shughuli zao za ujasiriamali na biashara.
- vi. Baadhi ya vikundi vya vijana kutofanya vizuri katika marejesho ukilinganisha na vikundi vya wanawake.
- vii. Idadi kubwa ya vikundi vya wanawake na vijana kuhitaji mikopo kuliko upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mifuko ya WDF na YDF.

## 5.0 Mafanikio Yaliyopatikana:-

- i. Kwa kipindi cha mwaka 2016/ 2017 Halmashauri ilichangia asilimia kumi (10%) ya Mapato ya ndani kiasi cha shilingi **40,000,000/=** (Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake 30,000,000/= na vijana 10,000,000/=)
- ii. Kupata Mkopo wa shilingi **20,000,000/=** Mwezi Machi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto na kiasi cha shilingi **11,000,000/=** toka Wizara ya Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera,Bunge,Kazi,Vijana,Ajira, na Walemavu
- iii. Uundaji na Uzinduzi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi ngazi ya Wilaya na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ngazi ya kata ambapo majukwaa hayo yamaeundwa katika Kata zote 17 za Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na vijiji 66 na vitongoji 19.Majukwaa haya yamewawezesha wanawake wengi kutambua fursa zinazowazunguka na kuomba mikopo ya WDF, kujitathmini, kueleza changamoto zao za kiuchumi pamoja na kupata elimu ya ujasiriamali, haki za kiuchumi , haki za wanawake na fursa ya kushiriki katika makongamano.
- iv. Kuongezeka kwa mtaji kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Walemavu kutoka shilingi **7,000,000/=** mwaka 2014/2015 hadi kufikia mtaji wa Milioni wa shilingi **147,500,000/=** hadi Novemba 2017. Kati ya Mtaji huo kiasi cha shilingi **20,000,000/=** ni kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Watoto na kiasi cha shilingi **18,500,000/=** Wizara ya Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Kazi, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu.Na mchango wa Halmashauri wa asilimia 10% ni shilingi **109,000,000/=**.
- v. Halmashauri ya Wilaya ina jumla ya vikundi vya uzalishaji mali vilivyotambuliwa 4,627 vyenye jumla ya wanachama 33,256. Kati ya vikundi hivyo 643 vimepata usajili Halmashauri sawa na asilimia 14%.Aidha,elimu ya ujasiriamali na biashara imetolewa kwa sehemu kubwa hali inayopelekea kujitokeza kwa vikundi vingi sana kuomba mikopo na kujitokeza kwa wingi kwenye makongamano ya ujasiriamali na biashara.
- vi. Kutengeneza jarida la vijana la Wilaya linaloonyesha kazi za uzalishaji mali zinazofanywa na vijana katika Wilaya yetu

- vii. Kuanzisha, kusimamia, na kushauri mchakato wa kuunda Saccos ya Wanawale ya Wilaya ambayo mpaka sasa wana mtaji wa shilingi **3,743,000/=** unaozunguka. Tayari wameanza kukopeshana wenyewe kwa wenyewe.
- viii. Mwamko mkubwa wa wanawake na vijana katika kuanzisha shughuli za uzalishaji mali na ujasiriamali, na kujiunga katika vikundi, pamoja na kuchangamkia fursa mbalimbali kama vile mikopo toka Mfuko ya mMaendeleo ya Wanawake (WDF), vijana (YDF), walemavu, mikopo toka taasisi za fedha, kujiunga kwa wingi katika vikundi vya kuweka Akiba, HISA na kukopeshana (VICOBA).
- ix. Kushirikiana na wadau kama PPF, Tanzania Women Bank (TWB), DCB, LAPF, TPB, TFDA, BRELA, TBS, SIDO kufanya makongamano ya wajasiriamali wanawake na vijana ambapo jumla ya wananchi 5,385 waliweza kufikiwa na kujengewa uwezo
- x. Kupita katika Kata zote 17 na kutoa elimu kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF), Vijana (YDF), na walemavu pamoja na elimu ya ujasiriamali, biashara na utunzaji wa kumbukumbu wa shughuli zao
- xi. Vikundi vingi vinavyokopeshwa vinaendelea kurejesha mikopo yao vizuri bila usumbufu ambapo mpaka sasa ni vikundi vichache sana vinasumbua kurudisha marejesho.

## **6.0 Mikakati ya Idara**

- i. Kuunganisha mifumo ya uhamasishaji jamii ili iweze kuamsha ARI ya ushiriki katika uzalishaji kwenye sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi ili kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa zinazozalishwa na kuwezesha upatikanaji wa malighafi zitakazotumika katika viwanda vidogovidogo, vya kati na vikubwa
- ii. Kuamsha ARI ya Jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo zitakazochochea uboreshaji wa huduma za jamii ikiwemo ujenzi wa miundo mbinu ya barabara, maji, afya, na elimu ili kufikia uchumi wa viwanda
- iii. Kuratibu na kuunganisha juhudi za wananchi/vikundi vya kiuchumi na Taasisi wezeshi kama vile VETA, SIDO, FDCs, BRELA, TBS, TFDA, CDTIs, taasisi za fedha na mifuko ya uwezeshaji kiuchumi ili ziweze kushirikiana na Halmashauri katika kuwajengea uwezo wananchi na vikundi vya uzalishaji kufikia Tanzania ya Uchumi wa Viwanda

- iv. Kuamsha ARI ya jamii kupiga vita mila potofu na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ili kuokoa fedha inayotumika kuhudumia wahanga wa ukatili na kuwawezesha kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa na rasilimali ziliopo katika kujenga uchumi wa viwanda
- v. Kuendelea kuomba fedha kutoka Taasisi nyingine za kifedha wezeshi ili kutunisha Mfuko huu ( Baadhi ya taasisi hizo ni kama vile TPB,DCB, PPF, LAPF, NMB, SELF,SIDO etc)
- vi. Halmashauri kuendelea kuchangia asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani na kulipa uzito suala la Mfuko wa Maendeleo ya wanawake (WDF), vijana (YDF) na walemavu ili kuvikopesha vikundi vingi zaidi.
- vii. Idara kuendelea kutunza takwimu za vikundi vilivyokwisha kupatiwa mikopo na kuendelea kuvitambua na kuvijengea uwezo vikundi vingine vyenye kuhitaji mikopo toka ngazi za vijiji na Kata
- viii. Kuendelea kufuatilia marejesho kutoka kwa vikundi vilivyokwisha kukopeshwa mikopo ili viwe vinarejesha kwa wakati
- ix. Kushirikiana na Taasisi za fedha wezeshi kama Benki za Dar e Salaam Community Bank ( DCB) , na Tanzania Postal Bank (TPB) kusimamia na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya wanawake,vijana, na walemavu.

## **7. TAARIFA YA ULINZI NA USALAMA WA MTOTO NA JITIHADU ZA KUPINGA UKATILI DHIDI YA WATOTO (VAC) KATIKA WILAYA YA KISARAWE.**

Katika kutekeleza ilani ya chama cha mapinduzi (ccm) na utekelezaji wa sheria ya mototo Na21 ya mwaka 2009, serikali ya awamu ya tano inaelekeza kusimamia upatikanaji wa haki za makundi maalum ikiwemo albino nawatoto waishio mitaani pamoja na kuanzisha kamati za ulinzi na usalama wa mototo katika halmashauri.

Halmashauri imetekeleza kwa kuunda Timu ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa ngazi ya wilaya ,kamati hii ilianzishwa rasmi mwaka 2014 chini ya ufadhili wa umoja wa nchi za ulaya (EU) kupitia shirika la UNICEF. Watekelezaji wa uundwaji wa kamati hii ni shirika la Plan



International tawi la Kisarawe kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe pamoja na shirika la ANNPCAN ambalo ni mshiriki mwenza wa Plan International.

### **Lengo Timu Ya Ulinzi Na Usalama Wa Mtoto**

Kupunguza Changamoto Za Kitendaji Katika Kupinga Ukatili Dhidi Ya Watoto kama mwongozo wa sheria ya mtoto wa mwaka 2012 inayoilekeza halmashauri kusimamia ulinzi na usalama wa mtoto kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama kwa mtoto na kutokomeza aina zote za ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto sambamba na utoaji elimu kwa jamii na kutambua athari za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

### **Hali halisi ya ukatili dhidi ya watoto kisarawe.**

Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vimekuwa vikifanyika ingawa vitendo hivyo haviripotiwi kwenye vyombo Husika. Utafiti juu ya ukatili dhidi ya watoto uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali linalohudumia watoto duniani (UNICEF) kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania ilibainisha kuwa kati ya watoto watatu (3) wa kike na mmoja kati ya saba (7) wa kiume wanafanyiwa aina moja wapo ya ukatili kabla ya umri wa miaka 18.

Katika wilaya yetu kulikuwa na matatizo mbalimbali ikiwemo ,mimba za utotoni,ndoa za kulazimishwa ukatili huo unabainisha kuwa kwa asilimia kubwa vitendo hivyo hufanyika zaidi katika mazingira ya nyumbani, shuleni na njiani. Takwimu zinaonyesha matukio haya hufanywa zaidi na watu wa karibu yao kama baba mama, mjomba n.k

Aidha,mbali na changamoto mbalimbali timu ya ulinzi na usalama wa mtoto imefanikiwa kuzuia kabisa watoto kuishi mitaani

### **Timu ya ulinzi na usalama wa mtoto**

Timu ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa ngazi ya Wilaya ambayo ina wajumbe 25 na inajumuisha idara mbalimbali ili kuweka msukumo na mkazo kwenye halmashauri juu ya ulinzi na usalama wa motto, timu hiyo inaundwa na wataalam wafuatao:-

- i. Afisa Ustawi Wa Jamii (W) - Mwenyekiti
- ii. Afisa ustawi - Katibu

- iii. Afisa Elimu Msingi (W)
- iv. Afisa Elimu Sekondari(W)
- v. Mganga Mkuu
- vi. Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
- vii. Hakim Mahakama Ya Watoto
- viii. Afisa Mipango,(W)
- ix. Polisi Dawati La Jinsia
- x. Mwasheria (W)

- Timu ilijengewa uwezo kupitia Maafisa ustawi wa jamii waliobobea kwenye ulinzi na usalama wa mtoto.
- Kutoa mafunzo ya jinsi ya kukusanya taarifa yalitolewa kwa timu za ulinzi na usalama wa mtoto na (WCPT na MVCC) pamoja na maafisa ustawi wa jamii wote walio ngazi ya wilaya na kata za mradi.
- Kujengea uwezo namna ya uendeshaji wa mahakama ya watoto kwa afisa ustawi wa mahakama na wadau wote wa mahakama yalifanyika.

#### **TAKWIMU ZA KESI ZILIZOFIKISHWA MAHAKAMANI KUANZIA 2015 HADI 2016**

AINA YA KESI	IDADI	KESI ZILIPOFIKIA	HUKUMU	
			Hukumu/ Fidia	Kushinda/Kuachiwa Huru
Ubakaji	21	Zimeisha	6(hukum30yrs)	15
Ukatili wa kimwili	-	-	-	-
Kesi nyingine	8	Zimeisha	3 (wamelipa fidia )	6
<b>Jumla</b>	<b>30</b>		<b>9</b>	<b>21</b>

#### **TAKWIMU ZA KESI ZILIZOFIKISHWA MAHAKAMANI KUANZIA 2016 JUNE HADI 2017 DESEMBA**

AINA YA KESI	IDADI	KESI ZILIPOFIKIA	HUKUMU	
			Hukumu/ Fidia	Kushinda/Kuachiwa Huru

Ubakaji	28	Zimeisha	3(hukum30yrs)	10
Ukatili wa kimwili	2	imeisha	kurejeshwa katika familia zao	-
Kesi nyingine	3	Zimeisha	3 (wamelipa fidia ,)	Ushaidi kushindwa kukamilika
<b>Jumla</b>	<b>33</b>		<b>7</b>	<b>21</b>

Kutokana na uelewa na mwamko wa wananchi idadi ya kesi inaonekana kuongezeka ingawa bado kunachangamoto za baadhi ya wanafamilia kumalizana nyumbani kindugu hii ufifisha ushaidi mahakamani na wengine kukana (turn hostile) wakati wa kusilizwa kwa shauri

### **Changamoto.**

- Uhaba wa fedha kuzitembelea timu za ulinzi ngazi ya kata na vijiji
- Watoto kuzungukwa na mazingira hatarishi kama vile kusoma shule za mbali na nyumbani, kuchota maji umbali mrefu na kutafuta kuni mbali na nyumbani hupelekea kufanyika vitendo vya kikatili..
- Kukosekana kwa ushahidi wa kesi za ubakaji inayopelekea watuhumiwa kuachiwa huru.

Timu hii ya ulinzi na usalama wa mtoto inafanya mengi ikiwemo kupinga ukatili dhidi ya watoto na imeonyesha kuwa na mafanikio makubwa sana katika wilaya yetu ya Kisarawe hususani kwenye kata na vijiji. Jamii imehamasika sana kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama wa watoto na wanatoa ushirikiano katika kukabiliana na kesi za ukatili dhidi ya watoto.

### **Hatua muhimu zinazochukuliwa na timu**

- i. Kufanya ushawishi kwa wadau mbalimbali kupunguza changamoto za watoto mashuleni na nyumbani
- ii. kuandaa mpango wa utekelezaji na ratiba za uhamasishaji
- iii. kuainisha rasilimali (resources) zitakazohitajika kwa wadau, taasisi na mashirika ya kuhudumia watoto

### **TAARIFA YA MFUKO AFYA WA JAMII (CHF)**

Mfuko wa Afya wa jamii CHF ni mpango wa hiari ulioanzishwa kwa sheria Na 1 ya mwaka 2001, (Sura 409), sheria za Tanzania toleo la mwaka (2002), wa kaya au familia kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua. Wanufaika wa mfuko huu ni pamoja na:-

- Baba, mama na mtoto chini ya umri wa miaka 18 au
- Mtu yoyote mwenye umri zaidi ya miaka 18 Au

- Tasisi, mfano shule (mwanafunzi),Ushirika (Wanaushirika ,Vikundi vya Uzalishaji Mali nk.)

Lengo la uanzishwaji wa mfuko wa afya ya jamii hapa Tanzania ni kuahakikisha wananchi wote ambao hawako kwenye ajira rasmi wanapaata mfuko ambao unawawezesha kupata huduma za afya ya msingi kupitia uchangiaji wao wa moja kwa moja.

Katika Halmashauri ya Kisarawe uchangiaji huo huduma kwa miezi kumi na mbili (12) kwa kiasi cha TSh. 10,000/= (Elfu kumi) ambapo watu 6 ndani ya kaya moja huhudumiwa na mfuko huo (baba, mama na watoto wane waliochini ya miaka 18).

- Utaratibu wa mtu kuwa/kujiunga na mfuko huo CHF ni kama ifuatavyo:-
  1. Kuchangia mwenyewe (wale wenye uwezo)
  2. Kaya maskini kuchangiwa na Serikali ya kijiji
  3. Wananchi kuchangia kupitia fedha zao za vikoba, malipo ya ruzuku kupitia mradiwa TASAF III.
  4. Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na watu binafsi kujitolea kuchangia kaya zisizojiweza.

### **Matibabu anayoweza kupata mwanachama wa (CHF)**

Mwanachama wa (CHF) anaweza kupata matibabu ndani ya hospitali ya Wilaya, Zahati na dispensary husika ndani ya wilaya (Kisarawe).

Mwanachama wa (CHF) anahaki ya kupata matibabu ya nje (OPD) mfano kumuona daktari, kupata vipimo vya maabara, (HB,MRDT,URINE NA STOO,) kung'oa meno, kusafisha vidonda na dawa.

### **MWOGOZO WA MATUMIZI YA FEDHA ZA CHF KWA MKOA WA PWANI**

Wizara ya Afya imetoa mwongozo wa fedha za uchangiaji wa huduma za Afya (NHIF,CHF,NA PAPO KWA PAPO) matumizi yote ya fedha hizo katika matumizi yanatakiwa kuzingatia mwongozo wa fedha hizo kama ifuatavyo:

- 67% Dawa
- 15% Vifaa tiba/Vitenganishi
- 18% Matumizi mengineyo kama motisha kwa watumishi, ukarabati mdogo mdogo na N.K.

### **MAFANIKIO YA MFUKO WA AFYA YA JAMII. (CHF)**

- Mpaka sasa tumefanikiwa kuwa na wanachama 424 sawa na asilimia 52%
- Tumesajiliwa na (SSRA) Mamlaka ya udhibiti wa mifuko ya Jamii
- Tumeweza kupata mkataba wa malipo ya fedha za tele kwa tele kutoka NHIF
- Tumefanikiwa kushughulikia madai ya fedha za tele kwa tele toka 2008 hadi 2017 na yapo katika mchakato wa malipo .

- Kupata wadau kutoka TASF ambao husaidia kaya masikini kwa kufadhili kaya Masikini CHF.
- Tayari kata 17 zimesha hamasishwa kupitia wadau mbali mbali.

### **CHANGAMOTO ZINAZOUKABILI MFUKO WA AFYA YA JAMII.**

- Uchache wa wachangiaji kulingana na hali ya maisha kuwa ngumu
- Uelewa mdogo kwa jamii juu ya mfuko wa Afya ya jamii.
- Bado jamii haijahasika katika ngazi ya kijiji.

### **HALI YA HUDUMA ZA AFYA WILAYANI KISARAWE**

Idara inatoa huduma kwa wakazi wa Kisarawe wapatao 114,054 ambapo wanawake ni 57,216 na wanaume ni 56,838.

Akina mama wenye umri wa kuzaa ni 25,668, watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja ni 3,159, watoto chini ya miaka mitano 11,769. Kwa mwaka 2016 kiwango cha vifo vitikanavyo na uzazi ilikuwa 174/100,000, vifo vya watoto chini ya miaka mitano ni 1/1000 na vifo vya watoto wachanga chini ya siku 28 ni 2/1000 na vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja 3/1000.

### **HALI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA.**

Sera ya afya ta mwaka 2007 inaagiza kila kijiji kuwa na Zahanati na kila kata kuwa na kituo cha afya. Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ina jumla ya vijiji 66 na vilivyo na Zahanati ni 27 sawa na asilimia 41%. Hivyo kuna upungufu wa Zahanati 39 sawa na upungufu wa asilimia 59%.

Halmashauri ina jumla ya kata 17 ambapo kati ya kata hizo kuna vituo vya Afya 4 ambavyo sawa na asilimia 24%. Upungufu wa vituo 13 sawa na asilimia 76%. Idara ya afya ina jumla ya watumishi 363 ikilinganishwa na uhitaji wa watumishi 645 hiyo kufanya upungufu wa watumishi kwa asilimia 64.

### **UPUNGUFU WA VIFAA TIBA**

Upungufu wa vifaa tiba kwa mwaka 2017/2018 ni asilimia 40%.

Kiwango cha upatikanaji wa dawa ni asilimia 83.6%.

### **HALI YA VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI**

Vimepungua mwaka hadi mwaka kwa mwaka **2016** 174/100,000 kulinganisha na mwaka **2015** – 182/100,000

Kiwango cha chanjo kwa **Penta3** ni 88%, **Surua** ni 94%, **Polio 0** ni 107%.

Vifo vya watoto chini ya miaka mitano ni 1/1000.

Kiwango cha vifo chini ya siku 28 (Neonatal death ni 2/1000).

Kiwango cha vifo vya watoto chini ya mwaka 1 (Infant mortality rate ni 3/1000).

### **HUDUMA YA MATIBABU KWA WAZEE**

Halmashauri ina jumla ya wazee 52,000 kati yao 3,500 wanaostahili kupata vitambulisho vya matibabu bila malipo. Wazee waliotambuliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu bila malipo ni wazee 2,229.

Kiwango cha utapiamlo wa kadri ni 12%

Kiwango cha utapiamlo mkali (SAM) ni 0.9%.

### **CHANGAMOTO ZINAZOKABILI IDARA YA AFYA:**

1. Uhaba wa watumishi wa idara ya afya kwa kiwango cha 64%
2. Bado kuna wajawazito wanaojifungulia majumbani
3. Upungufu wa vifaa tiba
4. Vituo vinavyopata maji kwa mwaka mzima ni 37%, 63% vinapata maji safi msimu wa mvua.
5. Upungufu wa vyumba vya kutolea huduma. Dispensing, Store ya dawa, chumba cha kupumzika mama baada ya kujifungua.
6. Upungufu wa vyumba vya Maabara.
7. Vifo vitokanavyo na uzazi – 174/100,000
8. Vifo vya watoto wa chini ya miaka mitano 1/1000
9. Vifo vya watoto wachanga(28day) – 2/1000.
10. Uhaba wa nyumba za watumishi kwa asilimia 69%
11. Ukosefu wa gari la usimamizi kwa CHMT

### **MKAKATI WA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOPO**

1. Halmashauri kuendelea kuomba vibali vya ajira kwa watumishi wa afya.
2. Kuongeza bajeti ya vifaa na fedha zinazopitishwa kwenye bajeti zinachelewa kupokelewa katika ngazi ya vituo na Halmashauri. Kuimarisha mfuko wa Bima ya Afya jamii ili kuongeza mapato na kusaidia kupunguza makali ya ufinyu wa bajeti
3. Kuendelea kuweka katika mipango ya bajeti na kushirikisha wadau wa maendeleo kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji safi katika vituo vya kutolea huduma.
4. Halmashauri kuendelea kuboresha miundombinu inayoendana na wakati uliopo.
5. (a) Kuendelea kukamilisha zahanati ambazo hazijakamilika:-  
(b) Kuboresha huduma za upasuaji wa dharura katika vituo vya afya kupunguza umbali wa kufuata huduma.  
(c) Kuendelea kutoa elimu katika ngazi mbalimbali za jamii na viongozi ili kutambua umuhimu wa kuwahi matibabu na kuanza kliniki mapema ili kuweza kupata

huduma mapema kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na mama wajawazito ili kupunguza vifo

- (d) Kuwepo na mfuko wa kijiji kusaidia wajawazito
  - (e) Kuimarisha mfumo wa rufaa kutoka ngazi zote .
6. Ukamilishaji wa zahanati uende sambamba na ukamilishaji wa nyumba za watumishi.
7. (a) Halmashauri kuweka kwenye mpango wa kununua gari kwa ajili ya usimamizi elekezi ili kufanya kazi kwa ufanisi.
- (b) Kuwasiliana na Wizara ya Afya na TAMISEMI kuomba gari kwa ajili ya usimamizi.